**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baiskeli Dar es Salaam**
**Tarehe 15 Septemba 2007**

**Waliohudhuria**
Ally Saidi Mohamedi
Ally Saidi Mwishehe
Elaine Baker
Filbert Mbecha
Izdoly Aludo Kihalule
Juma Ali Salehe Jongo
Kassim Bakari
Kibwana Mohammad Msiga
Musa Athumani Lahi
Mussa Omari
Patrick Maziku
Ramadhani Rajabu Nyengo
Sosthenes C Amlima
Sudi Saidi Ramadhan

**Msafara wa baiskeli**
Wakati wa wiki tuligundua kwamba tarehe 13 octoba pengine ingekuwa sikuku ya Idd. Hii ilisababisha mjadala ikiwa ingekuwa siku nzuri kufanya msafara kwani familia nyingi za kiislam zingekuwa zinasherekea. Elaine aliwasiliana na mbunge Azan Zungu ambaye alisema atakuwepo jumamosi itakayofuata ambayo ni tarehe 20. pia aliwasiliana na bwana mlamba wa AALOCOM na Jax wa CHABADA ambao walikubali tarehe 20 kwamba ni nzuri zaidi. Ingawa jax atakuwa mwanza kwenye mashindano yam bio za baiskeli ila wajumbe wa CHABADA watakuwepo. Elaine aliwatumia ujumbe mfupi wanachama wa UWABA na 11 walikubali ni bora tarehe 20, jumamosi.

Hivyo basi Juma alisambaza barua kwa mashirika yote tuliyoyashusisha kuwataarifu kuhusu mabadiliko ya tarehe ikiwemo wafadhili wetu. Bakhresa, kampuni ya Guta na Ubalozi wa china.

Kwenye mkutano ilikubalika kuhamisha tarehe hadi tarehe 20 na kutuma mialiko na barua ya mabadiliko ya tarehe kwa Ultimate Security, askari wa usalama barabarani, upendo Disabled sports club na walemavu Saccos karume.

Elaine alifuatilia barua Manispaa ya Ilala kuthibitisha kutumia Mnazi Mmoja na Mbunge Azan Zungu alimpa namba ya simu ya mtu anayehusika katika manispaa Ilala na Juma alipeleka barua huko kuomba barua thibitisho.

Baadhi ya watu waliripoti kwa wanachama wa UWABA kwamba mkutano wetu na waandishi wa habari umeonyeshwa usiku huo kwenye taarifa ya habari channel Ten.

Juma alipiga simu idara ya stoo ya Game aliambiwa arudi ijumaa itakayofuata wakati meneja husika atakapo kuwa amerudi.

Ilikubalika kutuma barua kuomba ufadhili CRDB, NBC, NMB banks kiwanda cha urafiki na Ubalozi wa Ireland.

Sosthenes alileta vibendera 12 vyenye kaulimbiu kadhaa vya kuweka kwenye baiskeli wakati wa msafara. Jumatatu Elaine na Juma walitoa na kumpa sosthenes Tsh 55,000 zaidi ili kutengeneza mabango makubwa ambayo hayako tayari.

Ilikubalika kwamba tuweke mabango ya matangazo kwenye shule na kuwahimiza wanafunzi washiriki.

Ally Mohammedi alipendekeza kwamba tutengeneze vipeperushi vyenye maelezo ili vigawanywe wakati wa msafara kuhusu faida za upandaji baiskeli na haki za wapanda baiskeli na usalama wa wapanda baiskeli hivyo hata washiriki ambao hawatashinda wataondoka na kitu chochote.

Ilikubalika kuchapa tiketi za bahati nasibu wenyewe badala ya kuzinunua. Ilikubalika kutumia fedha za UWABA kununua wino wa kuchapia kwa ajili ya mashine ya Elaine badala ya kupeleka sehemu nyingine kwani hii itasaidia uchapaji wa vitu vingine.

**Guta na Ofisi**

Jumanne amesafiri kwenda Tanga na Ally Saidi Mohamed ameumia mkono vibaya alianguka kutoka kwenye paa hivyo hakuna maendeleo yoyote ya ofisi wala guta. Jumanne atarudi wiki hii na Ally Saidi anategemea kuweza kufanya kazi na ndugu yake mdogo kutengeneza rafu ya magazeti

**TANROADS**

Juma alichukua barua kutoka TANROADS kujibu barua yetu jumatano kwa vile ni muhimu Elaine alitoa nakala na kuwapa wajumbe wote kwenye mkutano na kuiweka kwenye mbao ya matangazo. Barua ilikuwa inatia moyo kwa malengo yetu na kuonyesha kwamba TANROADS watapenda kushirikiana na UWABA. Walipitia maswali yetu na kujibu kila moja baadhi ya mambo chanya ni kwamba katika barabara za sam Nujoma na Kilwa, wataweka njia za wapanda baiskeli na mikokoteni zikitenganishwa na sehemu ya magari na waenda kwa miguu. Hata hivyo kwenye barabara ya Nelson Mandela kutakuwa na barabara za pembeni zitakazotumika kwa baiskeli, waenda kwa miguu na magari.

Wanachama walikuwa na nyongeza na huhitaji ufafanuzi zaidi

- barabara za pembeni zimetajwa kwenye barua – je zimetenganishwa na eneo la waenda kwa miguu na wapanda baiskeli au ni moja?
- Je ni vizuizi gani vitawekwa kuzuia magari makubwa kuingia eneo la wapanda baiskeli, barabara za maegesho. Je kingo za barabara zilizotajwa zinalinda sehemu ya wapanda baiskeli au za waenda kwa miguu tu?
- Je eneo la baiskeli liko kushoto au ni katikati ya eneo la waenda kwa miguu na barabara kuu.?

- Je ni hatua gani zitachukuliwa kuhakikisha barabara inatunzwa (hasa alama za barabarani, taa za mitaani) baada ya ujenzi kukamilika?
- Kutakuwa na eneo la biashara kama fundi baiskeli na vioski vidogo ambavyo havizibi njia?

Wajumbe waliridhika kupokea majibu kutoka TANROADS kwa maandishi kwamba watafuatilia utekelezaji kwa mipango ya baadaye.

Ilikubalika kuitisha mkutano na TANROADS tarehe 26 ili tuwaeleze mambo haya kwao

**Vitambulisho**
Paulo alitengeneza vitambulisho na kumkabidhi Elaine kwani hakuweza kuhudhuria mkutano wa leo. Elaine alileta vitambulisho ambavyo havijawekwa karatasi ngumu na baadhi ya wanachama walisaini vitambulisho vyao ili vikamilishwe na Paulo wiki ijayo. Wengine waliomba vitambulisho vya aina nyingine.

**T-Shirts**
Meja hakuweza kuhudhuria mkutano leo lakini ametuma mfano wa T-shirts aliyotengeneza. Wanachama walizipenda na wakapendekeza nyuma ya Tshirt kuwe na maneno "Thamani Baiskeli"yanayomaanisha kwamba baiskeli ni muhimu na inatakiwa kuheshimiwa. Neno UWABA pia lichapwe nyuma ya T-shirt. Ilikubalika pia kwamba mbele neno "Dar es Salaam" kwani hilo ni sehemu ya jina la kiofisi la UWABA.

**Kituo cha daladala Mwenge**
Juma alipeleka barua kwenye Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni kuomba ufafanuzi kuhusu baiskeli katika kituo cha Daladala mwenge. Elaine alipigiwa simu na mtu kutoka manispa lakini simu ilikatika kabla hajamaliza kuongea. Alisema lengo letu kuu ni kupata ufafanuzi kuhusu sera gani inayohusu wapanda baiskeli kituoni hapo.

**Ukubwa wa baiskeli**
Robert Bartlett wa ujerumani alitupa njia ya mawasiliano wa mhandisi kutoka Benin, Badji Placide ambaye anafanya utafiti vipimo vya guta. Tulipima na kumpa maelezo.

**Bike Art Nouveau, Milan, Italia**
Piergiorgio petruzzellis wa lastazione delle bicicleltewa millan, Italia wametumia barua pepe kutuarifu kwamba wanafanya maadhimisho ya baiskeli mwezi huu yaitwayo Bike Nouveau fabric na wamepanga kufanya mnada wa baiskeli zilizotengenezwa kwa mkono (zilizotengenezwa wakati wa maadhimisho (kama sehemu ya mashindano) ili kusaidia kazi zifanywazo na UWABA. Wanachama walifurahi kusikia haya na Elaine aliwatuma maelezo na picha za UWABA.